

Shairi la Mtoto hana salala limeandikwa na Mshairi Bakari Mwamboga wa Uholanzi, likiwa jibu lake kwa shairi la Mheshimiwa Yusuf Kalala juu ya shairi lake katika Toleo la 4. la Diwani ya Tanzanet, Januari - April 2003. Linazungumzia malezi kwa watoto.

MTOTO HANA SALALA

- | | |
|--|---|
| <p>1. Ulosema nayapinga, ndugu Yusufu Kalala,
Lea mwana kwa kupanga, mwana asipate ila,
Kuchapa juwa kwa nonga, utamtia madhila,
Mtoto hana salala, utoto sio ujinga,</p> | <p>5. Awe mwana wakuranga, hasomi hafungi sala,
Umkanyapo apinga, heshi baghala bughula,
Kwa ujana kujiringa, sijambo la kuduala,
Mtoto hana salala, utoto sio ujinga</p> |
| <p>2. Kesho wajazua janga, kimuumiza ghafula,
Uanze kutanga tanga, kiguu kila mahala,
Utamaliza waganga, hutakula hutalala,
Mtoto hana salala, utoto sio ujinga,</p> | <p>6. Akichelewa wafunga, nyumba yako hata lala,
Mtoto unamtenga, asipawe hata kula,
Hufunzi wamvononga, ufanyavyo si kimila,
Mtoto hana salala, utoto sio ujinga</p> |
| <p>3. Wameshasema wahenga, kulijibu hili swala,
Mwana ni kama mpunga, nafaka tunayo kula,
Kuna mchele na chenga, majaliwa yake Mola,
Mtoto hana salala, utoto sio ujinga ujinga.</p> | <p>7. Mzazi wewe ni kinga, wajibu kakupa Mola,
Mtoto hajawa bunga, mlinde kila pahala,
Mwana akijiviringa, muonye yake maswala,
Mtoto hana salala, utoto sio ujinga</p> |
| <p>4. Kupiga kuna visanga, chungu waja fungwa jela,
Mtoto wajamgonga, aanguke kwa ghafula,
Hasira zitakuzonga, mwana ende na machela,
Mtoto hana salala, utoto sio ujinga</p> | <p>8. Tamati natia nanga, si mche mwana kwa jala,
Peleleza na kupanga, mambo yote kwa jumla
Mkono utakufunga, kulea sikutawala,
Mtoto hana salala, utoto sio ujinga</p> |

B. Mwamboga
Holland, 31.07.03
